

# Anoka-Hennepin

## Kitabu cha Elimu Maalum



ANOKA-HENNEPIN

SCHOOLS

*A future without limit*

# Yaliyomo

Ni nini Elimu Maalum .....	3
Sehemuza Ulemavu.....	3 - 4
Misingi(ABCs)ya Elimu Maalum.....	5
Mchakato wa Elimu Maalum.....	6
Vipengele vya IEP.....	7
Kurasa za timu ya IEP.....	8 - 9

Mpendwa Mzazi/ Mlezi,

Hongera Hongera kwa kuchukua hatua kubwa kuelekea kumsaidia mtoto wako kujifunza.

Tunajua kila mtoto hujifunza kwa njia tofauti. pia tunajua kwamba ingawa kuomba na kupokea msaada wakati mwingine ni vigumu; pia ni jambo la ujasiri sana, na litamsaidia mtoto wako anapoitia katika shule.

Tunajua kuwa kila mtu anaingia katika elimu maalum kutoka mahali tofauti. iwe mtoto yupo katika umri wa mapema au shule ya sekondari, tunatumai mwongozo huu utakusaidia kuelewa wafanyakazi wapya na maneno ambayo ni sehemu ya elimu

Tumeandaa Mwongozo huu kwa

Katika safari hii, tunakuhimiza kupata njia za kutetea haki za mtoto wako. Zungumza na walimu kuhusu kile kinachofanya kazi kile kinachoweza kuboreshwa. Unafahamu mtoto wako vyema zaidi, na unajua nguvu na udhaifi wake. Wewe ni mmoja wa timu ya elimu maalum ya mtoto wako, na sauti yako ni muhimu.

Usiogope kuzungumza na kuuliza maswali.

Kutakuwa na nyakati ngumu, lakini unafanya vizuri. **Kweli. Unafanya vizuri.**

Pamoja Katika hili

*Kamati ya Ushauri ya Elimu Maalum (SEAC)*

Kamati ya Ushauri ya Elimu Maalum (SEAC) ni ushirikiano kati ya wilaya ya shule na wazazi/malezi wa wanafunzi wa Anoka-Hennepin wenye ulemavu. Kikundi hiki hukutana mara nne kila mwaka wa shule na kinawakilisha aina mbalimbali za ulemavu, na kinatumika kama mdhamini wa programu za elimu maalum zenye ubora wa juu. unaweza kujifunza zaidi kuhusu kikundi hii kwa kutembelea <https://www.ahschools.us/domain/173>.

**Daima unakaribishwa kwenye mikutano yetu**

### **Baadhi ya maoni kutoka kwa wazazi wa SEAC:**

"Nimekuwa wakilishi wa mzazi katika kamati ya Ushauri ya SEAC kwa miaka mingi na nimefurahia sauti yangu kusikika katika kushiriki mawazo kusaidia kuboresha huduma za darasa, msaada na makubaliano kwa watoto wetu wenye mahitaji maalum. Ninathamani maoni na maarifa niliyojifunza kutoka kwa wazazi wengine amabo pia wako katika kamati ya ushauri ya SEAC, na ni jambo zuri kujua kwamba hatuko peke yetu katika kutetea elimu ya watoto wetu. Pia imekuwamuhimu kwangu kujua kile wafanyakazi wa elimu maalum wa Anoka-Hennepin hufanya kila mwaka kutoamazingira bora ya kujifunzaiana ujumuishaji kwa watoto wetu. Ningependekeza sana kuhusika na kamati ya SEAC ili uwe kati ya wengine wanaoelewa safari yakoya kutaka elimu bora kwa watoto wenye mahitaji maalum ya kujifunza. *Cindy, Special Education Parent*

"Mtoto wangu alianza shule katika Anoka-Hennepin katika darasa la kwanza. Shule ilikuwa nzuri sana katika kumpa huduma na kutoa msaada ili awe na mafanikio. Binti yangu alianza kwenye IEP mwishoni mwa darasa la pili na sasa yupo darasa la nane. Niliingia katika kamati ya Ushauri ya Elimu maalum mwaka wa 2019. Ninatoa shukrani kwa wilaya na kile tulichokipata kupitia kamati hiilo mekuwa jambo zuri kufahamiana na wazazi wengine na kujifunza jinsi wilaya inavyolenga kukidhi kila mwanafunzi mahali alipo na kuwasaidia kufikia malengo yao" - *Sara, Special Education Parent*

"Watoto wangu wamekuwa katika Shule za Anoka-Hennepin tangu mwaka wa 2013 na nimekuwa nikihisi kila wakati kwamba viongozi wa shule walikuwa na maslahi bora ya watoto wangu moyoni Wavulana wangu wadogo wana IEP, hivyo nilijuanga na kamati ya Ushauri ya Elimu maalum mwaka wa 2019. Nimevutiwa na jamii ya wazazi na wafanyakazi wa wilaya wanaofanya kazi za kuunda zana za kuwapa wanafunzi katika wilaya yetu nafasi bora ya kukua kitaaluma na kijamii. Pia nilifurahia kukutana na wazazi wengine katika wilaya yetu, kuwa marafiki nao, na kufanya maamuzi yanayowapa watoto wetu wote kila fursa ya kufanikiwa." - *Amanda, Special Education Parent*

# Elimu Maalum ni nini?

Chini ya Sheria ya Elimu kwa Watu Wenye Ulemavu (IDEA), elimu maalum inamaanisha:

*"Maelekezo yaliyoundwa maalum, bila gharama kwa wazazi, ili kukidhi mahitaji ya kipekee ya mtoto mwenye ulemavu. Watoto wanaopokea elimu maalum na huduma zinazohusiana wana haki ya kupata elimu ya umma bure na inayofaa (FAPE). Hii ni pamoja na fursa ya kushiriki katika mtaala wa kawaida wa shule na kufanya maendeleo kuelekea kufikia malengo ya kila mwaka. Watoto wanaopokea elimu maalum pia lazima wawe na fursa ya kushiriki katika shughuli nyingine za kawaida za shule ambazo zinaenda na mahitaji yao binafsi."*

Huko Minnesota, shule zinahitajika kutoa huduma kwa watoto wanaostahiki kuanzia kuzaliwahadi umri wa miaka 21, au hadi kuhitimu shule ya pili, kulingana na ambayo itatokea kwanza. Huduma hizi hutolewa na wafanyakazi waliothibitishwa na zinajumuisha ufundishaji maalum, vifaa, na mbinu za kipekee.

## Shule za Anoka-Hennepin zinawapa wanafunzi wenye mahitaji ya elimu maalum fursa ya kupata huduma zinazofaa katika maeneo yafuatayo ya ulemavukama inavyofafanuliwa na idara ya Elimu ya Minnesota:

- **Autism Spectrum Disorder (ASD):** Kundi la matatizo yaliyoelezwa kwa tabia, yanayoonyeshwa na maendeleo yasiyo sawa na muundo wa upungufu wa ubora katika mwingiliano wa kijamii, mawasiliano, na mifumo ya tabia, maslahi na shughuli zinazojirudia na za kawaida, ikianza wakati wa utoto
- **Kupoteza Uone-Kipungufu cha Kuona(BVI):** Kipungufu cha kuona kilicho thibitishwa kiasya kinacholingana na vizuizi vya kuona vinavyoshindwa kupata taarifa au kuingiliana na mazingira kiasi kwamba mafunzo ya elimu maalum na huduma zinazohusiana ni muhimu.
- **Kiziwi- Kipofu(DB):** Inajumuisha kipungufu cha kusikia na kuona, mchanganyiko wake unasababisha mahitaji ya mawasiliano na mahitaji mengine ya maendeleo na elimu.
- **Kiziwi-Kiufundi cha kusikia(DHH):** Upungufu wa hisia za kusikia, au kupoteza kusikia kunavyoonyeshwa kwa vipimo vya kawaida vya sauti.
- **Kipungufu cha Kimaendeleo cha Akili(DCD):** Uwezo wa akili wa jumla ulio chini sana kuliko wastani, unaosababisha au unaohusiana na upungufu katika tabia za kujiendesha: iwe, Hafifu hadi Wastani au Kina-Kikubwa.  
**Kuchelewa Kimaendeleo (Elimu maalum ya Utoto wa Mapema, Kuzaliwa-Miaka 7 tu):** Kuchelewa kubwa au tatizo katika maendeleo au hali inayoonekana ya hisia, kimwili, kiakili, kijamii/kihisia, au hali nyingine zinazojulikana kuzuia maendeleo ya kawaida
- **Tatizo la Hisia/Tabia(EBD):** Muundo uliowekwa wa mwingiliano unaoonyeshwa na moja au zaidi ya yafuatayo:
  - tabia za uchokozi mkali sana
  - tabia za kutenda bila kufikiria
  - tabia za kujitenga kupita kiasi
  - tabia za wasiwasi
  - hali ya huzuni inayoenea kwa ujumla
  - huzuni
  - mabadiliko makubwa ya hisia
  - michakato ya mawazo iliyoharibika sana inayoonekana kupitia mifumo isiyo ya kawaida ya tabia mitindo ya mawasiliano isiyo ya kawaid, au mahusiano yaliyopotoka kati ya watu

- **Ulemavu Mwingine wa Afya (OHD):** Aina apana ya hali za kiafya sugu zilizohibitishwa kitabibu pamoja na hali za ghafla zinazohusiana nazo, amabazo huathiri vibaya utendaji wa kielimu kiasi kwamba elimu maalum na huduma zinazohusiana zinaweza kuhitajika
- **Ulemavu wa Kimwili (PI):** Ulemavu wa kimwili wa muda mrefu uliohibitishwa kitabibu, wa kuzaliwa au uliopatikana baadaye, unaoathiri vibaya uwezo wa kimwili au utendaji wa kitaaluma.
- **Ulemavu Mkubwa wa Nyingi (SMI):** Mwanafunzi ana matatizo makubwa ya kujifunza na maendeleo yanayotokana na hali mbili au zaidi za ulemavu
- **Ulemavu Maalum wa Kujifun za(SLD):** Hali ambapo kuna tofauti kubwa kati ya uwezo wa jumla wa kiakili wa mtu na mafanikio yake ya kitaaluma katika eneo moja au zaidi ya yafuatayo:
  - kujieleza kwa mdomo
  - kusikiliza ufahamu
  - hesabu za kihisabati
  - hoja za kihisabat
  - stadi za msingi za kusoma
  - kusoma ufahamu
  - maelezo ya maandishi
- **Matatizo wa Usemi/Lugha (SLI):** Tatizo la mawasiliano katika ufasaha, sauti, matamshi au lugha
- **Jeraha la Ubongo la Kiwewe (TBI):** eraha la ubongo lililopatikana linalosababishwa na nguvu ya kimwili ya nje,linalosababisha ulemavu wa jumla au wa sehemu katika utendaji au upungufu wa kisaikolojia/kijamii, au vyote viwili,unaoathiri vibaya utendaji wa kielimu wa mtoto

## Huduma Husika,za moja kwa moja na zisizo moja kwa moja ni nini?

### Huduma za Elimu Maalum Hutolewaje?

Huduma za moja kwa moja hutolewa moja kwa moja kwa mwanafunzi na mtaalamu. Huduma zisizo za moja kwa moja hutolewa na mtaalamu kwa mwalimu, wazazi, au wengine wanaofanya kazi moja kwa moja na mwanafunzi. Huduma zisizo za moja kwa moja zinaweza kujumuisha ushauri, mapitio ya maendeleo pamoja na timu ya IEP, uchunguzi, na kujadili mikakati ya kumsaidia mwanafunzi kufanya kazi vizuri zaidi.

Ingawa lengo ni wanafunzi kufundishwa katika shule iliyo karibu na makazi yao, si kila wakati inafaa kulingana na mahitaji binafsi ya mwanafunzi. Wanafunzi wanaweza kuwekwa katika programu inayoweza kushughulika mahitaji yao maalum. Mahitaji ya kitaaluma, ya kiutendaji, na ya kitabia katika programu hizi yanaweza kutofautiana, na yanaweza kuendeshwa sambamba na elimu ya kawaida, huku kuongeza ushirikishwaji katika madarasa ya kawaida ukiwa lengo.Baadhi ya wanafunzi huonyesha mahitaji makubwa zaidi kuliko yale yanaayoweza kutolewa katika shule ya kawaida au tovuti ya kawaida Wanafunzi hawa wanaweza kupokea huduma zao katika kituo cha kujifunzia cha River Trail, ambacho ni kituo cha elimu maalum

### Huduma Zinazohusiana ni nini?

Huduma zinazohusiana ni huduma za msaada au shughuli zinazohitajika kwa baadhi ya wanafunzi wenye ulemavu ili kuboresha matokeo yao ya kielimu. Timu ya IEP huamua kama huduma inayohusiana ni muhimu kusaidia malengo na madhumuni ya IEP ya mwanafunzi. Huduma hizi zinazohusiana zinaweza kuwa za moja au zisizo za moja kwa moja.Huduma zinazohusiana zinaweza kujumuisha, lakini hazizuliwi kwa:

- tiba ya kazi (OT)
- Tiba ya zoezi ya mwili
- huduma za kisaikolojia
- huduma za afya shuleni
- huduma ya muuguzi shuleni
- huduma za tiba ya usemi na lugha
- usafiri
- huduma za mwelekeo na uhamaji
- elimu ya viungo vya maendeleo na urekebishaji

Baadhi ya huduma zinazohusiana haziwezi kutolewa kama huduma ya pekee. ili kupokea msaada wa baadhi ya huduma hizi, mwanafunzi lazima awe anastahiki huduma za elimu maalum chini ya ulemavu wa msingi tofauti na ule wa usemi nalugha.

# Msingi (ABC) ya Elimu Maalum

<b>ADA</b>	Sheria ya Wamerakani Wenye Ulemavu	<b>IDEA</b>	Sheria ya Elimu kwa watu wenye ulemavu
<b>ASD</b>	Spektramu ya wigo wa Autism	<b>IEP</b>	Mpango/Programu ya Elimu ya kibinafsi
<b>ASL</b>	Lugha ya Ishara ya Marekani	<b>IHP</b>	Mpango wa Afya ya Kibinafsi
<b>AT</b>	Usaidizi wa Teknolojia	<b>IFSP</b>	Mpango wa Huduma Maalum kwa Familia
<b>BIP</b>	Mpango wa uingiliaji wa tabia	<b>LAUNCH</b>	Wanafunzi wenye Mahitaji ya Autism na Changamoto za Kipekee
<b>BIS</b>	Mtaaalamu wa Uingiliaji wa Tabia	<b>LEA</b>	Wakala wa Elimu wa Mitaa
<b>BVI</b>	Uoni hafifu/Kipofu	<b>LEP</b>	Uwezo mdogo wa lugha ya Kingereza
<b>CM</b>	Msimamizi wa Kesi	<b>LRE</b>	Mazingira yenye Vizuizi Vichache
<b>CST</b>	Timu ya utafiti wa mtoto	<b>OT</b>	Tiba ya kazi
<b>DAPE</b>	Elimu ya viungo iliyorekebishwa kwa maendeleo zaidi	<b>PCA</b>	Msaidizi wa utunzaji wa kibinafsi
<b>DB</b>	Kiziwi-Kipofu	<b>PI</b>	Wenye Ulemavu wa Kimwili
<b>DCD-MM</b>	Ulemavu wa Utambuzi wa Maendeleo Kiasi hadi Wastani	<b>PLAAFP</b>	Viwango vya Sasa vya Mafanikio ya Kitaaluma na Utendaji wa Kawaida
<b>DCD-SP</b>	Ulemavu wa Utambuzi wa Maendeleo Mkali/kubwa sana	<b>PT</b>	Tiba ya Mwili
<b>DD</b>	Kuchelewa kwa Maendeleo	<b>SEAC</b>	Baraza la Ushauri la Elimu Maalum
<b>DDH</b>	Kiziwi na mwenye Upungufu wa Kusikia	<b>SLD</b>	Ulemavu maalum wa Kujifunza
<b>EBD</b>	Matatizo ya Hisia au Tabia	<b>SLP</b>	Mtaaalamu wa Usemi na Lugha
<b>ECSE</b>	Elimu maalum ya utotoni	<b>Ulemavu mkubwa sana</b>	
<b>EIP</b>	Programu wa Uingiliaji wa Mapema	<b>SMI</b>	
<b>EL</b>	Mwanafunzi wa Kiingereza	<b>TBI</b>	Jeraha la Ubongo Linalosababishwa na Mshtuko
<b>ESY</b>	Mwaka wa Shule Uliiongezwa	<b>TSES</b>	Mfumo jumla wa Elimu maalum
<b>FAPE</b>	Elimu ya Umma ya Bure inayofaa		
<b>FBA</b>	Tathmina ya Tabia na utendaji		
<b>FEDERAL SETTING</b>	Kiasi cha Muda mwanafunzi anachotumia katika Elimu maalum		
	I = 0-21%		
	II = 21-60%		
	III = 60% au zaidi		
	IV = tovuti tofauti ya elimu maalum		
	V = hospitali, matibabu ya mchana au kituo		

# Mchakato wa Elimu Maalum wa Anoka-Hennepin



Mchakato wa kuingia na kutoka katika elimu maalum unapaswa kufafanuliwa wazi kwa pande zote ili kufikia suluhisho bora kwa familia.

Walimu au wazazi wanatambua kwamba mwanafunzi wao anakabiliwa na changamoto darasani. Timu inayojumuisha wazazi na wataalamu hukutana pamoja na kubuni mapendekezo ya hatua za uingiliaji zinazotekelezwa darasani.

1  
HELP  
NEEDED

Tathmini itajumuisha kupima ujuzi wa mwanafunzi katika maeneo yote yanayohusu. Inaweza kujumuisha mifano ya kazi, vipimo, uchunguzi darasani, pamoja na mahojiano na wazazi na walimu.

2  
REFERRAL

Tathmini itajumuisha ukaguzi wa ujuzi wa mwanafunzi katika maeneo yote yanayohusiana. Inaweza kujumuisha sampuli za kazi, vipimo, uchunguzi wa darasa, pamoja na mahojiano na wazazi na walimu.

3  
EVALUATION

Ndani ya siku 30 baada ya kuthibitishwa kufaa, Mpango/ Mfumo wa Elimu Binafsi (IEP) unaandikwa.

Mpango huo utaeleza malengo/ makusudio na kueleza msaada wowote wa ziada unaohitajika na mwanafunzi kufanikisha.

Pia utaeleza mazingira yasiyo na vikwazo vya ziada (LRE) kwa mwanafunzi pamoja na huduma zake.

INDIVIDUALIZED  
5  
IEP  
EDUCATION PLAN

4  
ELIGIBILITY

Timu itakutana na kupitia taarifa

zilizokusanywa wakati wa tathmini na kubaini kama mwanafunzi anastahiki elimu maalum na anahitaji mafunzo maalum.

Mwanafunzi atapokea huduma zake kama zilivyoelezwa katika IEP yake. Maendeleo yake yatafuatiliwakwa karibu na kuripotwa kwa mzazi/mlezi mara kadhaa kila mwaka.

6  
SERVICES

IEP lazima ipitiwe upya na kusasishwa na timu angalau mara moja kwa mwaka. Mwanafunzi lazima afanyiwe tathmini upya angalau mara moja kila baada ya miaka 3.

7  
REVIEW

8  
EXITING  
SPECIAL  
ED

Wanafunzi wanaokidhi malengo yao na ambao hawahitaji tena mafundisho maalum hupimwa na kuondolewa katika huduma za elimu maalum.

Sheria ya Elimu kwa Watu Wenye Ulemavu (IDEA) ni sheria ya shirikisho inayotoa miongozo na kanuni kuhusu jinsi majimbo na mashirika ya umma yanavyotoa huduma za kuingilia mapema, elimu maalum, na huduma zinazohusiana. Idara ya Elimu ya Minnesota (MDE) inatoa miongozo na kanuni za ziada

# Vipengele vya Mpango wa Elimu

<p><b>Mwaliko Rasmi</b></p> <hr/> <p>Timu ya shule itakuuliza kuhusu siku na muda</p> <p>unaofaa na itatumia nyumbani mwaliko rasmi wa mkutano.</p>	<p><b>Fomu ya Kujiandikisha ya Mkutano wa Timu</b></p> <hr/> <p>Kila mtu anayehudhuria mkutano atajitambulisha</p> <p>na kujiandikisha</p>	<p><b>Kuachishwa kwa Mwanachama wa Timu</b></p> <hr/> <p>Kama mwanachama wa timu hawezi kuhudhuria mkutano kwa sababu yoyote ile, timu itakuomba ruhusa yako kuachisha mwanachama huyo kwa kutoa sahihi kwenye fomu ya kujiandikisha</p> <p>Hii inatoa ruhusa ya mkutano kufanyika bila huyo mtu.</p>	<p><b>Viwango vya Sasa vya Mafanikio ya Kitaaluma na Utendaji wa Kawaida</b></p> <hr/> <p>Timu itakuomba maoni ya mzazi kuhusu nguvu, udhaifu, na maeneo yanayohitaji kutiliwa maanani ya mwanafunzi.</p>
<p><b>Malengo ya mwaka</b></p> <hr/> <p>Wanachama wa timu watajadili malengo na madhumuni wanayopendekeza kwa mwaka. Haya yanatengenezwa kwa maoni ya mzazi.</p>	<p><b>Malazi na Marekebisho</b></p> <hr/> <p>The team will discuss what accommodations and modifications may be needed in the general classroom.</p>	<p><b>Mwaka wa Shule Uliongezwa (ESY)</b></p> <hr/> <p>Timu itajadili kama huduma za mwaka wa shule uliopanuliwa zinahitajika..</p>	<p><b>Programu na Huduma</b></p> <hr/> <p>Huduma mbalimbali zitatumika kujadili ili kubaini ni ipi inayofaa zaidi na mazingira yasiyo na vikwazo vingi (LRE) kwa mwanafunzi kufanya maendeleo.</p>
<p><b>Tathmini</b></p> <hr/> <p>Kama mwanafunzi anashiriki katika vipimo vya darasa, wilaya, na/ au kitaifa, hivyo vitajadiliwa, pamoja na marekebisho yoyote.</p>	<p><b>Mpango wa Kuingilia Tabia (BIP)</b></p> <hr/> <p>Kama tabia ya mwanafunzi inaathiri ujifunzaji wake, basi Mpango wa Tabia ya Kila Mwanafunzi (BIP) utajadiliwa.</p>	<p><b>Sehemu ya Mpito ya IEP</b></p> <hr/> <p>Sehemu ya mpito ya IEP itajadiliwa kabla au wakati wa mwaka wa 9 wa mwanafunzi.</p>	

IE zinaundwa kwa juhudi za pamoja za timu. Daima toa wasiwasi na maoni yako. Mipango hii ni sahihi kwa mwaka mmoja, na timu hukutana kila mwaka. abari za maendeleo ya malengo zitatumiwa nyumbani kwa ratiba iliyowekwa mapema (kawaida mwishoni mwa robo au kipimo ha muhula).

ama mabadiliko yanahitajika kabla ya timu kukutana kila mwaka, wazazi wanaweza kuomba mkutano wa IE ili kujadili marekebisho ya mabadiliko yanayo aa.



**Ni kina nani hawa watu wote?  
Kwa nini wote wako hapa?  
Wanafanya kazi gani?**

Katika kila mkutano wa IEP lazima kuwe na:

**1**

Wazazi au walezi wa kisheria

**2**

Mwallimu wa elimu ya kawaida (General education teacher)

**3**

Mwalimu wa elimu maalum (Special education teacher)

**4**

Mwakilichi wa wilaya ya shule (District representative)

**5**

Mtu anayeweza kutafsiri au kuelezea matokeo ya tathmini

**6**

Mwanafunzi (ikiwa inafaa)

Wakati minginge mtu mmoja anaweza kuwa na majukumu zaidi ya moja katika mkutano wako, na mkutano wako unaweza kuwa na watu wachahe kama 3 tu. Hakikisha unajua nani atakuwepo kabla hujaenda!

**Katika Shule za Anoka-Hennepin, wanafunzi wataanza kualikwa kuanzia Darasa la 9.**

## MWALIMU WA ELIMU YA KAWAIDA

Huyu ndiye mtu kwenye timu yako anayehusika na kufundisha mtoto wako darasani kila siku. Hii ni pamoja na kubadilisha kazi za darasa ili mwanafunzi wako aweze kushiriki na wenzake.

Mwalimu wa darasa lako ni:

\_\_\_\_\_

Unaweza wasiliana nao:

\_\_\_\_\_

## MWALIMU WA MASOMO MAALUM

Huyu ndiye mtu kwenye timu yako anayehusika na kutimiza mahitaji ya kujifunza ya mtoto wako binafsi. Hii inaweza kujumuisha kufanya kazi za hesabu, kusoma, kuandika, na ujuzi wa kijamii kwa kutumia mbinu maalum za ufundishaji.

Mwalimu wako wa masomo:

\_\_\_\_\_

Unaweza wasiliana na:

\_\_\_\_\_

## MTAALAMU WA TIBA YA USEMI NA LUGHA

Huyu ndiye mtu kwenye timu yako anayehusika na kutimiza mahitaji ya mawasiliano ya mtoto wako. Hii inaweza kujumuisha kufanya kazi juu ya jinsi mtoto wako anavyoongea au kuelewa na kutumia lugha.

SLP wako ni:

\_\_\_\_\_

Unaweza wasiliana nao:

\_\_\_\_\_

## MWANASAIKOLOJIA WA SHULE

Huyu ni mtu katika timu yako anayehusika na kutathmini afya ya akili, ujifunza na tabia, haswa wakati wa tathmini. Hii inaweza kujumuisha kusimamia vipimo vya uwezo wa kiakili au mafanikio ya kitaaluma, kupima na kufasiri tathmini za wazazi na walimu, au kufanya mahojiano

Mwanasaikolojia wako ni:

\_\_\_\_\_

Unaweza wasiliana nao:

\_\_\_\_\_

## MTAALAMU WA TIBA YA KAZI

Mtaalamu wa Kazi (OT) ndiye mtu kwenye timu yako anayehusika na kutimiza mahitaji ya motor ndogo, maisha ya kila siku, na hisia za mtoto wako. Hii inaweza kujumuisha kufanya kazi juu ya mambo kama uandishi wa mkono, kufunga vitufe, au kudhibiti hisia binafsi.

OT wako ni:

\_\_\_\_\_

Unaweza wasiliana nao:

\_\_\_\_\_

## MTAALAMU WA TIBA KAZI THIPRA RIOT

Huyu ndiye mtu kwenye timu yako anayehusika na kutimiza mahitaji ya ujuzi wa harakati ya mwili.

Hii inaweza kujumuisha kupanga Ziada za Michezo ya Mwili (Adaptive PE) na kufanya kazi juu ya kusimama, kutembea, au kazi nyingine za kimwili.

Mwanatherapia wako ni:

\_\_\_\_\_

Unaweza wasiliana nao:

\_\_\_\_\_

## MWAKILISHI WA WILAYA

Mtu huyu ndiye anayehusika na kuwasilisha uwezo na vikwazo vya wilaya ya shule.

Hii inaweza kujumuisha kutoa taarifa na kujibu maswali kuhusu huduma za elimu maalum, marekebisho, na uelewa wa rasilimali zinazopatikana katika wilay.

Msimamizi wako ni:

\_\_\_\_\_

Unaweza wasiliana nao:

\_\_\_\_\_

## WAJUMBE WENGINE WA TIMU

Kulingana na mahitaji ya mtoto wako, unaweza kuwa na watu wengine kwenye timu yako. Hawa wanaweza kujumuisha mtu kama mtaalamu wa kuingilia tabia, mtaalamu wa kusikia na viziwi, au wengine..

Wako \_\_\_\_\_ ni:

\_\_\_\_\_

Unaweza wasiliana nao:

\_\_\_\_\_

Wako \_\_\_\_\_ ni:

\_\_\_\_\_

Unaweza wasiliana nao:

\_\_\_\_\_

Wako \_\_\_\_\_ ni:

\_\_\_\_\_

Unaweza wasiliana nao:

\_\_\_\_\_